MAMBO 10 AMBAYO HUKUJUWA KUHUSU BENKI YA DUNIA

VIPAUMBELE VYA BENKI YA DUNIA VIMEBADILIKA MNO

Katika mwaka wa 1980, uwekezaji katika sekta ya umeme ulichukuwa asilimia 21 ya mikopo ya Benki. Kwa wakati huu kiasi hicho kimefikia karibu na asilimia 7. Hata hivyo, usaidizi kwa afya, lisho bora, elimu, fedha za kustaafu, na huduma nyengine za kijamii umeongezeka kutoka asilimia 5 katika mwaka wa 1980 hadi asilimia 22 hivi leo. Benki, ambayo inamilikiwa na mataifa 184, inafanya maendeleo kwa namna tofauti na inashughulikia maswala mapya zaidi kama vile ya isimu, maendeleo yanayoelekezwa na jamii, jamii za asili, pamoja na kufanya kazi ya kuhakikisha kuweko kwa misingi ya muhimu kwa watu masikini.

1. Benki ya Dunia ni mfadhili mkubwa zaidi wa nje wa elimu

Tangu usaidizi wake wa elimu uanze mwaka wa 1963, Benki ya Dunia impeana kiasi cha bilioni $31 za Kimarekani kama mikopo na karadha, na kwa sasa inadhamini miradi 158 ya elimu katika nchi 83. Benki hufanya kazi kwa karibu na serikali za kitaifa, mashirika ya Umoja wa Mataifa, wafadhili, mashirika yasiyokuwa ya kiserikali, na washirika wengine katika kusaidia nchi zinazoendelea katika juhudi zao za Kutimiza malengo yao ya Elimu kwa Wote. Malengo haya yanahakikisha kuwa watoto wote-haswa wasichana na watoto wanaotoka kwenye jamii zenye shida-wanakwenda shule na wanaweza kukamilisha masomo ya msingi ikifikia mwaka wa 2015. Mfano mzuri wa mikopo ya Benki ya elimu ni katika India District Primary Education Program [Mradi wa India wa Elimu ya Msingi Wilayani], ambayo lengo lake ni watoto wakike katika wilaya ambazo idadi ya wanawake wanaojuwa kusoma na kuandika iko chini ya kiwango cha taifa. Udhamini wa Benki katika mradi huu sasa umefikia bilioni $1.3 za Kimarekani na unawafaidi zaidi ya wanafunzi 60 milioni katika wilaya 271 zenye idadi ya chini ya wanao juwa kusoma na kuandika katika majimbo 18 kati ya 29 ya India. Brazil, El Salvador, na Trinidad and Tobago, miradi ya Benki inaunga mkono shughuli za jamii za karibu za kuboresha elimu kwa kuwapa ruhusa ya kuwakifia mafanikio ya shule na walimu wa sehemu zao.

2. Benki ya Dunia ni mfadhili mkubwa zaidi ulimwenguni katika vita dhidi ya HIV/UKIMWI

Kila siku, watu, 14,000 zaidi wanaambukizwa viini vya HIV; nusu yao wakiwa ni wa umri wa kati ya miaka 15 na 24. HIV/UKIMWI inarudisha nyuma kwa upesi sana mengi kati ya mafanikio ya kiuchumi na kijamii yaliyopatikana na nchi zinazoendelea kwa mda wa miaka 50 iliyopita. Ikiwa mdhamini mshiriki wa UNAIDS—ambayo huendesha hatua za ulimwengu za kutatua mkasa huu—Benki ya Dunia imehakikisha kuweko kwa mchango wake zaidi ya $1.7 bilioni za Kimarekani katika juhudi za kukinga kuenea kwa HIV/UKIMWI duniani. Benki imeahidi kwamba hakuna nchi yenye mbinu za kufaa za kupambana na HIV/UKIMWI itakayokosa kupata msaada. Na katika juhudi za kushirikiana na serikali za Afrika, Benki ilianzisha Multi-Country HIV/AIDS Program (MAP) [Mradi wa Ukimwi kwa Mataifa Tofauti] ambayo huchangia kwa rasilimali zake kwa jumuiya hiari za wananchi na jamii. Nyingi kati ya jumuiya na jamii hizi zimeanzisha mbinu za uvumbuzi za kukabiliana na HIV/UKIMWI, na ambazo zimeanza kuigwa na mataifa mengine na kutekelezwa katika miundo ya jamii zao. Katika mwaka wa 2002, MAP ilipeana $1 bilioni za Kimarekani kuzisaidia nchi za Afrika kupanua miradi yao ya uepushaji, ukaguzi na matibabu. Benki pia iliidhinisha $155 milioni kukabiliana na HIV/UKIMWI katika Caribbean na inaendelea na juhudi zake za kuisaidia miradi ya HIV/UKIMWI katika sehemu nyengine.

3. Benki ya Dunia ni mojawapo ya wafadhili wakubwa wa nje wa miradi ya afya duniani

Kuhakikisha kuwa watu masikini wanapata huduma njema ya afya na lisho bora ndiyo kiini cha juhudi za kupunguza umasikini na kuchangia kukuwa kwa uchumi. Ingawa hatua kubwa zimefanyika katika nchi nyingi katika karne chache zilizopita, bado kuna vikwazo vikubwa. Kati ya watoto milioni 11 wanaokufa kila mwaka kwatika nchi zinazoendelea, kama asilimia 70 wanakufa kutokana na magonjwa ya kuambukiza (kwa mfano: homa ya bombo, kuhara, malaria, ukambi, na HIV/UKIMWI) na ukosefu wa lisho bora. Benki ya Dunia hutoa kiasi cha bilioni $1 za Marekani kwa mikopo mipya kila mwaka kwa kushughulikia afya, lisho bora, na miradi ya ongezeko la watu katika nchi zinazoendelea. Fedha za Benki zinasaidia kukabiliana na malaria katika nchi 46 na

katika vita dhidi ya kifua kikuu katika nchi 30. Katika Uchina, Benki imesaidia kupanwa kwa chumvi yenye madini kwa zaidi ya jamii asilimia 90. Hii inamaanisha kuwa kuna visa vichache zaidi vya kuharibika kwa mimba, vifo vya watoto baada tu ya kuzaliwa, kasoro za maumbile, na kutokomaa akili ambako husababishwa na ukosefu wa madini katika chumvi. Benki pia inasaidia akina mama wa Senegal kuepusha na kutibu ukosefu wa lisho bora kwa watoto na pia inasaidia katika juhudi za pamoja za kuepusha na kutibu magonjwa ya watoto Brazil.

4. Benki ya Dunia inatilia mkazo upunguzaji wa madeni

Katika mwaka wa 1996, Benki ya Dunia na International Monetary Fund (IMF) [Shirika la Kimataifa la Fedha] zilianzisha Heavily Indebted Poor Countries (HIPC) Initiative [Hatua ya Nchi Zenye Madeni Makubwa]—mbinu ya kwanza ya kupunguza madeni la kigeni ya nchi masikini zaidi na zenye madeni makubwa zaidi ulimwenguni. Leo, nchi 26 zinapata kupunguziwa madeni yanayo kadiriwa kufikia $40 bilioni za Kimarekani. Pakiwemo namna nyengine za kupunguza madeni,hatua ya HIPC itashusha madnei ya kigeni ya nchi hizi kwa thuluthi mbili na hivyo kupunguza kudaiwa kwao kufikia kiasi cha chini kwa jumla ya kile cha kawaida cha nchi zinazostawi. Sehemu nyengine ya mpango huu ni kuwa nchi hizi zinafanya mabadiliko katika mahitaji yao ya bajeti kwa kutilia maanani zaidi sekta muhimu za kijamii na maendeleo ya umma. Rwanda, kwa mfano, ina nia ya kuongeza idadi ya wanafunzi wanao jisahili shuleni na pia kuajiri walimu wengi zaidi. Honduras ina mpango wa kuwaifaidi anagalau watu 100,000 katika sehemu zenye umasikini mkubwa kwa kupeana huduma muhimu ya afya ya uzazi na ya watoto wachanga. Cameroon, rasilimali zinatumiwa kutilia mkazo vita dhidi ya HIV/UKIMWI kwa kusambaza elimu ili kuelimisha juu ya umuhimu wa kutumia mipira ya kukinga maradhi ya zinaa haswa kati ya watu wenye athari kuu zaidi ya kuambukizwa ugonjwa.

5. Benki ya Dunia ni mojawapo ya wafadhili wakubwa zaidi wa kimataifa wa miradi ya mali ghafi

Tangu mwaka wa 1988, Benki imekuwa mojawapo ya wafadhili wakubwa zaidi wa kimataifa wa miradi ya mali ghafi. Hata ingawa kupotea kwa mali ghafi ni jambo linalo shughulisha ulimwengu, hasara kubwa zaidi wanaiona wakazi wa sehemu za mashambani katika nchi zinazoendelea, ambao wanategemea kwa wingi zaidi mazingira yao kwa chakula, ujenzi wa makao, madawa, ujira na pia kwa utamaduni. Kwa sababu hii, Benki imejuinga na Conservation International [Udumishi wa Kimataifa], Global Environment Facility [Jumuiya ya Ulimwengu lya Mazingira], MacArthur Foundation [Hazina ya MacArthur], pamoja na serikali ya Ujapani katika kuanzisha hazina itakayo changia ulinzi mwema wa sehemu za mali ghafi za nchi zinazoendelea. Asilimia sitini ya mali ghafi ya viumbe vya ardhini inapatikana katika sehemu hizi zenye kuathiriwa, ambazo zinaukubwa wa asilimia 1.4 ya ardhi yote. Wasiwasi kuhusu mazingira ni sehemu kiini ya juhudi za Benki za upunguzajii wa umasikini. Mbali na ukaguzi wa mazingira na sera za uhifadhi, mbinu mpya ya mazingira inajishughulisha na mabadiliko ya hali ya anga, misitu, rasilimali za maji na mali ghafi. Kwa wakati huu, hazina ya Benki yenye malengo muhimu ya mazingira ina kiwango cha $14 bilioni.

6. Benki ya Dunia hufanya kazi kwa ushirikiano kwa wingi zaidi kushinda zamani

Kwa miaka sita iliyopita Benki ya Dunia imejuinga na washirika wa aina mbalimbali katika juhudi za kuuangamiza umasikini ulimwenguni: kwa mfano, imejiunga na World Wildlife Fund [Hazina ya Ulimwengu ya Pori] kwa kuhifadhi misitu, na pamoja na sekta ya umma na ya kibinafsi kwa kuanzisha Prototype Carbon Fund [Hazina Asili ya Kaboni] kusaidia kupunguza madhara ya kuingia joto dunia. Benki inashirikiana pia na Food and Agriculture Organization (FAO) [Shirika la Chakula na Ukulima] na United Nations Development Programme (UNDP) [Programu ya Umoja wa Mataifa ya Maendeleo] ilikufadhili Consultative Group on International Agricultural Research [Mshikano wa Mashauri ya Utafiti wa kimataifa wa Ukulima]—ambao hutilia makazo utumizi wa sayansi ya kisasa zaidi ukupunguza njaa na umasikini, kuboresha lisho bora na afya, pamoja na kuhifadhi mazingira. Kwa kushirikiana na Consultative Group to Assist the Poorest (CGAP) [Mshikano wa Mashauri ya Msaada kwa Mafukara] Benki inashughulika na wafadhili na taasisi za fedha kuimarisha uwezo wa taasisi ndogo za fedha kupena huduma kwa watu masikini. Ushirikiano wakuangamiza upofu unaotokana na maji ya mtoni umefaulu kuzuia matukio 600,000 ya upofu. Ushirikiano huu umeanzisha hekta milioni 25 za ukulima na kila mwaka hutibu watu zaidi ya milioni 22.

7. Benki ya Dunia ni kiongozi katika vita dhidi ya ufisadi ulimwenguni

Ufisadi ni kikwazo cha maendeleo: huwapa dhiki masikini inapotumia vibaya rasimali zilizopangiwa wanao zihitaji zaidi. Tangu mwaka wa 1996, Benki imeanzisha zaidi ya miradi 600 ya kuondoa ufisadi na kuimarisha utawala katika zaidi ya nchi wateja 100. Juhudi hizi ni kama: watumishi wa umma kuelezea mali wanayoimiliki, mafunzo na tarjisi ya mahakimu pamoja na kuwafunza waandishi wa habari mbinu za ukusanyaji habari kupitia uchunguzi. Karibu robo ya miradi mipya sasa inajuisha matumizi ya fedha za umma na namna za mageuzi ya kifedha. Juhudi za Benki za kuangamiza ufisadi imesaidia sana kuvutia mshiko wa ulimwengu katika juhudi hii. Benki ya Dunia inashughulika kujumuisha kikamilifu uongozi wa serikali na mbinu za kuangamiza ufisadi na mipango ya uendeshaji wa serikali. Benki imejitolea kuhakisha kwamba miradi inayo fadhili haikumbwi na ufisadi. Miaka minne iliyopita, Benki imeimarisha mbinu za kuhakisha kutokuwapo ufisadi pamoja na kuwekwa kwa mpango wa simu za malalamishi dhidi ya ufisadi. Kufikia Julai 2002, Benki ilikuwa imetangaza kuwa makampuni na wahusika 77 kuwa hawastahili kupata kandarasi zinazofadiliwa na Benki.

8. Utumishi wa umma unajukumu kubwa zaidi katika shughuli za Benki

Zaidi ya thuluthi tatu za miradi ya maendeleo iliyoidhinishwa na Benki katika mwaka wa fedha uliopita ulijumuisha ushirikiano wa nongovernmental organizations (NGO) [mashirika yasiyokuwa ya kiserikali] katika utekelezaji wake, na nyingi kati ya miradi yake imefaidika na mashauri ya utumishi ya umma. Benki sasa ina wafanyikazi katika ofisi za nchi 70 ulimwenguni. Wafanyikazi hawa pia hushirikiana na mashirika yasiyokuwa ya kiserikali katika miradi aina mbalimbali, kwa mfano: elimu, UKIMWI na mazingira. Katika Asia ya Kusini, Benki inafanya mashauri na utumishi wa umma kuhusu mambo ya jinsia, katika Ulaya ya Mashiriki kwa usaidizi wa baada ya vita na usimamizi wa serikali, na katika Amerika ya Kusini, Benki inashughulikia kupeana uwezo na mageuzi. Timor ya Mashirika ni mfano mzuri wa ushirikiano ambapo kupeana uwezo kwa jamii na Mradi wa Serikali za Mikowa zinasaidia mabara ya vijiji yaliyochaguliwa kwa demokrasia na yenye kujumuisha vijana, wanawake na vikundi vya kanisa na wakulima katika urekebishaji wa barabara, miradi ya maji, na kuanzisha upya miradi ya shughuli za kiuchumi kwa kupitia miradi ya jamii.

9. Benki ya Dunia husaidia nchi zilizokumbwa na vita

Kwa sasa Benki inafanya kazi katika nchi 40 zilizokumbwa na mikasa ya vita kwa kuchangia juhudi za kimataifa za kusaidia jamii zilizokumbwa na vita, kurudia maendeleo ya wakati wa amani, na kuepusha kurudia hali ya vita. Benki hushughulikia mahitaji ya aina mbalimbali zikiwemo juhudi za kufufua uchumi, uwekezaji katika sehemu zilizokuwa na vita, kurekebisha majengo na vifaa vilivyoharibika kwa vita, pamoja na kusaidia makundi kama ya wajane na watoto walioathiriwa na vita. Benki pia husaidia juhudi za kuondoa silaha, kusaidia makundi ya wapiganaji kujiunga tena na jamii, kutafuta mabomu ya ardhini, pamoja na kuwaelimisha watu. Kati ya miradi mbalimbali inayofadhiliwa na Benki ni: urekebishaji wa majengo na vifaa Afghanistan, kuwasaidia watoto wa mitaani wa Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Congo, shughuli za maendeleo ya mijini kusini mwa Serbia, mafunzo ya wafanyikazi wa serikali wa Timor ya Mashariki, na umoja wa kitaifa na kuhusisha jamii katika miradi Haiti.

10. Benki ya Dunia inasikiza maoni ya masikini

Mazungumzo na watu masikini 60,000 katika nchi 60, pamoja na kazi zetu za kila siku kumetufunza kwamba umasikini siyo tu ukosefu wa pato la kutosha ama hata maendeleo duni, bali pia ni kuhusu kutokuwa na sauti, kutoweza kujiwakilisha. Umasikini unahusu pia ufisadi na kuwa katika hali ya kudhulumiwa. Kutokuwa na haki ya utendaji, kuamua na kutokuwa na nafasi ya kujiendeleza. Tunaamini kuaa watu wanoishi katika hali za umasikini

hawastahili kuchukuliwa kuwa mzigo bali ni wenye thamani ya kuweza kuchangia kwa wingi zaidi ya wengineo katika kuangamiza umasikini. Kuukabili umasikin kwa kuwapa watu uwezo ni hatua ya kuwashirikisha kwa ndani zaidi masikini na huwezesha masikini wa kike na wakiume kuwa na mwongozo mwema zaidi maishani mwao kwa kupata maarifa, kushirikishwa, kuhudumiwa kwa uaminifu na kujishirkisha katika sehemu zao. Kwa wakati huu Benki inasaidia miradi inayoendeshwa na jamiii kwa kutoa michango ya zaidi ya bilioni $2.2. Huko Indonesia, vijiji 15,000 na vikundi vya mitaani vinaandaa mbinu zao wenyewe za kupata udhamini wa sehemu zao, ili hali huko Benin, wanawake wanashirikiana katika kuhifadhi misitu ilikuifanya chanzo za mapato na wala sio za kuni.